**HOTUBA YA MWENYEKITI WA BODI MAMA ANNE MAKINDA WAKATI WA UZINDUZI WA MKUTANO WA WATOA HUDUMA WA MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA, TAREHE 7 DISEMBA 2017.**

- Wajumbe wa Bodi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya,
- Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Bwana Benard Konga,
- Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam,
- Waganga Wakuu wa Wilaya za Mkoa wa Dar es Salaam,
- Viongozi wa Taasisi mbalimbali za Afya na Jamii mliopo hapa,
- Wakurugenzi wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya,
- Ndugu Watoa huduma,
- Ndugu Wanahabari,
- Mabibi na Mabwana,

Habari za Asubuhi.

Awali ya yote napenda kuwapongeza wote kwa uwepo wenu mahali hapa asubuhi ya leo lakini pia nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema na kutuwezesha wote kufikia siku hii salama.

**Ndugu Mganga Mkuu wa Mkoa na Watoa huduma wote,** nafasi hii ni muhimu sana kwangu hasa nikizingatia kwamba hii ni mara yangu ya kwanza kukaa pamoja na watoa huduma wa Dar es Salaam katika mkutano kama huu. Naithamini sana nafasi hii na kuienzi.

Natambua umuhimu mkubwa wa kundi hili kwa Mfuko huu na napenda kwa dhati kabisa kutoa pongezi kwenu kwa kuendelea kuwahudumia wanachama wa NHIF bila kuchoka. Ni dhahiri kuwa, ninyi ndio mnatoa

huduma kwa wanachama wetu, pamoja na changamoto nyingi ambazo zimekuwa zikijitokeza, nina wiwa kuwapongeza kwa kazi kubwa mnayofanya kwa kushirikiana na Mfuko huu hapa Dar es Salaam.

**Ndugu Mganga Mkuu na watoa huduma wote**, ni jambo lililo wazi kwamba uelewa wa dhana ya Bima ya Afya miongoni mwa Watanzania walio wengi umeongezeka sana ukilinganisha na miaka ya nyuma na hivyo kuongeza namba ya wanachama ambao wanapata huduma katika vituo vyenu vya kutolea huduma za matibabu kupitia bima ya afya.

Ongezeko hili linawataka ninyi kuongeza ubunifu wa namna ya kupunguza msongamano wa wanachama wa Mfuko huu wakati wanapokuja kupata huduma za matibabu vituoni mwenu lakini pia kuboresha zaidi huduma zenu ili kuondokana ama kupunguza malalamiko ambayo yamekuwa yakitolewa kila kukicha. Nimeshuhudia kwenye vituo vingi, takriban asilimia 80 au zaidi ya wagonjwa wanafika katika vituo vyenu kupata huduma ni wanachama wa NHIF. Kuna haja ya kuwa na mkakati madhubuti wa kulisimamia suala hili ili kuwa na ufanisi.

Kuongezeka kwa idadi ya wanachama, uboreshaji wa vituo vya kutolea huduma kupitia mikopo ya vifaa tiba na ukarabati wa majengo, uboreshaji wa mifumo ya utendaji kuitia TEHAMA na uamuzi wa kusogeza huduma kwa wanachama kwa kufungua ofisi za Mfuko katika kila mkoa Tanzania Bara na Zanzibar (**ugatuzi**) ni baadhi ya mafanikio ya Mfuko ambayo nanyi mnaweza kujivunia. Mafanikio haya yanatakiwa yalindwe na yaendelezwe daima.

**Ndugu Mganga Mkuu wa Mkoa na watoa huduma,** wakati tukijiandaa kuelekea hatua ya kila Mtanzania kuwa na Bima ya Afya kama matazamio ya Serikali yalivyo, mnalo jukumu la kuhakikisha mmejipanga na kuweka misingi imara ya utoaji wa huduma kupitia bima za afya kwa Watanzania wote tena kwa haraka sana.

Mfuko unalo lengo la kufikia asilimia 75 ya Watanzania wote ifikapo mwaka 2020, ambapo kwa sasa umefikia asilimia 31.5. Kuna haja kubwa ya kuhakikisha changamoto zilizopo sasa tunazimaliza ili kuweza kukabili idadi kubwa ya wanachama kwa siku za usoni. Lengo hilo linaweza tu kufikiwa iwapo huduma za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kupitia ninyi watoa huduma zitaendelea kuboreshwa hasa katika kipindi hiki ambacho Serikali kupitia Wizara imeendelea kuweka nguvu nyingi katika uboreshaji wa huduma za matibabu hasa suala la upatikanaji wa dawa.

Siku zote huwa si rahisi kumfunza anayezama jinsi ya kuogelea na mwenye macho haambiwa tazama. Ni vema tujipange ili mabadiliko yajapo tuwe tuko tayari kuhudumia bila kuwa na changamoto kubwa. Nasisitiza hili nikitazama kuwa kwa wingi wa vituo vya huduma vilivyopo hapa Dar es Salaam, na kwa uhuru ambao mwanachama wa NHIF anao kuchagua mahali pa kupata huduma, sina shaka kuna baadhi ya vituo kutokana na huduma nzuri wanazotoa vitakuwa na mlundikano mkubwa wa wanachama wakati vituo vinavyobaki nyuma na kutoa huduma zisizoridhisha zikikimbiwa.

**Ndugu Mganga Mkuu wa Mkoa na Watoa huduma**, Kumekuwa na tatizo la kuwa na lugha tofauti kati ya Mfuko na watoa huduma wakati wanachama wa NHIF wanapofika kwenu kupata huduma hatua inayosababisha malalamiko mengi na kuharibu kazi kubwa inayofanywa.

Kupitia kikao hiki, nawaomba kwa pamoja muwe wawazi katika masuala yote muhimu ambayo yamekuwa yakisababisha malalamiko mengi ikiwemo kutotolewa kwa baadhi ya dawa ama vipimo kwa wanachama na kauli ambayo imekuwa ikijirudia mara kwa mara ni kwamba "…… huduma hii hailipiwi na NHIF….." Ni matumaini yangu kuwa mkutano huu utajadili changamoto hizi na kuzipatia suluhu ili mkitoka hapa mkalete mabadiliko ya kihuduma kwa wanachama wa Mfuko kwa manufaa ya pande zote mbili.

**Ndugu Mganga Mkuu wa Mkoa na Watoa huduma,** Katika kuchangia maendeleo ya sekta ya afya nchini, tangu mwaka 2007 Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya umekuwa ukitoa mikopo nafuu ya vifaa tiba na ukarabati wa majengo kwa watoa huduma waliosajiliwa na Mfuko huu. Mikopo hii imekuwa ni msaada mkubwa na inategemewa kuendelea kuwa msaada kwa vituo katika kuboresha huduma wanazotoa kwa wananchi. Nitumie fursa hii pia kuwahamasiaha kuendelea kutumia fursa hii ili huduma za matibabu ziendelee kuimarika.

**Ndugu Mganga Mkuu,** tangu kuanzishwa kwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Serikali imekuwa na matarajio makubwa kwa Mfuko huu katika kutekeleza sera ya uchangiaji wa huduma za afya nchini na kama mlivyomsikia wenyewe Rais Dkt. John Pombe Magufuli ambavyo ameendelea kuhamasisha wananchi kutumia Mfuko ikiwa ni njia bora ya kupunguza gharama za matibabu hivyo pia kwa upande wetu ni lazima tujipange kuhakikisha huduma zinatolewa kwa ubora zaidi na kwa lugha yenye staha.

Kabla sijahitimisha niwaombe wote kutumia muda huu vizuri ili mkiondoka hapa kuwe na mafanikio kwa ajili ya wanachama wetu na mimi binafsi kama Mwenyekiti wa Bodi niko tayari kupokea maoni yoyote ambayo yana lengo la kujenga na kuimarisha Mfuko huu.

Baada ya kusema hayo machache sasa natamka kuwa mkutano huu umefunguliwa rasmi.

**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**